

# HALMASHAURI YA MJI WA KIBAHA



## ZABUNI YA UENDESHAJI WA MGAHAWA KITUO KIKUU CHA MABASI KIBAHA MJI

13/09/2018

**Tenda Na. LGA- 011/2018-19/HQ/NC/14**

### TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Mji wa Kibaha inakaribisha maombi ya Zabuni toka kwa Makampuni yenye sifa stahiki na uwezo kisheria kufanya kazi ya huduma ya uwakala wa Uendeshaji wa Mgahawa uliopo katika kituo kikuu cha mabasi kibaha mji, kwa kipindi cha kuanzia tarehe 01/10/2018 hadi tarehe 30/09/2019.

Barua za maombi ziambatanishwe na maelezo kamili na vivuli (vilivyothibitishwa) vifuatavyo:-

1. Leseni (halali) ya Biashara husika.
2. Hati ya kuandikishwa kwa Kampuni
3. Stakabadhi uliyolipia Ada ya Maombi ya Zabuni
4. Maelezo ya kazi ulizowahi kufanya na uzoefu usiopungua miaka miwili wa huduma ya Uendeshaji wa Mgahawa na Vielelezo vilivyothibitishwa na Waajiri wa awali kwa kazi husika.
5. Usajili wa TIN
6. Usajili wa VAT (*Kama inahusika*).
7. Uthibitisho wa ulipaji Kodi (*Tax Clearance Certificate*) ya mwaka 2016/2017
8. Muombaji ataje kiasi cha Fedha atakachowasilisha Halmashauri ya Mji kwa kila Mwezi ikizingatiwa kuwa Eneo kusudiwa lina Ukubwa wa mita za mraba 95.1 ( square mitre).

9. Muombaji aonyeshe idadi ya Wafanyakazi/Watendaji wake pamoja na sifa za Kitaalumu, Uzoefu/Ujuzi na Maadili ya kazi ya Huduma ya Uendeshaji wa Mgahawa [uthibitisho unahitajika].
10. Uthibitisho wa uwezo wa Muombaji kifedha kwa kuonyesha *Taarifa ya Fedha ya Benki (Bank Statement)* ya miezi mitatu ya hivi karibuni iliyoidhinishwa na kuthibitishwa na *Meneja wa Tawi la Benki husika*.
11. Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (*Power of Attorney*) wa mtu atakayehusika na Zabuni hii.
12. Muombaji aoneshe Taarifa za Hesabu za Kampuni za miaka miwili (2) hadi mitatu (3) iliyomalizika kabla ya kuomba Zabuni hii zilizokaguliwa na kuthibitishwa na Mkaguzi wa Hesabu (*aliyethibitishwa – Certified Public Accountant/Auditor*).
13. Taarifa ya madeni yake yote [kama yapo] anayodaiwa na watu binafsi, Benki au Taasisi nyingine.

Mzabuni mwombaji anatakiwa kulipia Ada ya zabuni kiasi cha Shilingi Laki Moja tu (100,000/=) ambayo haitarudishwa, pia Zabuni itakayowasilishwa bila kukamilika itaondolewa katika hatua za awali. **”Pre- Bidding Visit”** itafanyika tarehe 19/09/2018 saa Nne Asubuhi ikifuatiwa na kikao cha Majadiliano.

Mwisho wa kurudisha maombi ya zabuni ni tarehe **26/09/2018** saa **4.00** asubuhi siku ya Jumatano ambayo ufunguzi utafanyika. Juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja aina ya Zabuni, Namba ya Zabuni. Zabuni hizo zipelekwe katika sanduku la Zabuni lililopo Ofisi ya **Afisa Ugavi wa Mji** kwa kutumia anwani ifuatayo:-

**Mkurugenzi wa Mji, Halmashauri ya Mji wa Kibaha, S.L.P. 30112, KIBAHA.** Zabuni itakayochelewa haitafunguliwa. Kabrasha la Zabuni linapatikana Ofisi ya **Manunuzi na Ugavi**, kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni. Mwombaji/Mwakilishi anaruhusiwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni utakaofanyika tarehe 26/09/2018 saa 4.00 asubuhi, kwenye Ukumbi wa Mikutano Halmashauri ya Mji.

kwa maelezo zaidi wasiliana na Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Mji wa Kibaha. Aidha, tangazo hili linapatikana kupitia tovuti ya Halmashauri ambayo ni **www.kibahatc.go.tz**

*JENIFA C. OMOLO*  
**MKURUGENZI HALMASHAURI**  
**MJI KIBAHA**

